

# Ukweli wa Injili

Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa  
Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote

## KUWEKA WACHUNGAJI WAKFU

Kuwekwa wakfu kwa wachungaji ni jambo ambalo lilitikuwako katika kanisa la kwanza, na pia ni jambo ambalo linastahili kufanyika kwa njia ambayo inalingana na mfano ambaao umetolewa katika Agano Jipy. Lakini katika historia ya kanisa jambo hili limewahi kufanywa kulingana na vishawishi nya kisiasa—maanake likafanywa kwa njia mbaya ya kupotosha. Lakini hivi si kusema kwamba kanisa linastahili kuacha kufuata mafundisho ambayo yanafaa na taratibu ambazo zinafaa za kuweka wakfu wachungaji.

### Nini Maana ya Kuweka Wachungaji Wakfu

Wahudumu wa Injili, ambaao ndio wafanyi kazi shambani mwa Bwana, wanastahili kuwa watu ambaao wamechaguliwa na Bwana, na kupakwa mafuta za nguvu na mamlaka yake. Tendo la kuweka wakfu wachungaji ni tendo ambalo linakubaliana na mafundisho ya biblia. Pia, hili ni jambo ambalo hufanywa hadharani, kwa njia ya wachungaji wengine (ambao tayari wamewekwa wakfu) kumwekelea mikono mchungaji mpya ambaye amechaguliwa na kuhitimishwa na Roho Mtakatifu. Kulingana na maelezo ya kamusi ya lugha ya Kiyunani, *kamusi ya Thayer*, kuweka wakfu ni “kusimamisha mahali pake; kumweka mtu juu ya wale wengine, kumchagua mtu ili aongoze ofisi fulani, kuweka kitu mahali pake, kuunda, kutangaza.”

Katika utaratibu wa kanisa kumweka mchungaji wakfu ni jambo ambalo huleta maana na tangazo kwamba mtu huyo amechaguliwa na kuitwa katika huduma ya kanisa. Na kwa njia ya kuwekewa mikono na wachungaji wengine wa kanisa hilo, ambaao tayari washawekwa wakfu hapo mbeleni, hii inakuwa njia rasmi na inayokubaliana na maandiko ya kutambua wito na kuhitimu kwa mchungaji huyo mpya.

Mtume Paulo alimwandikia Tito na kumwambia, “Kwa sababu hii nalikuacha Krete, ili uyatengeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru” (Tito 1:5). Tito aliendelea kukaa Krete ili kufuatilia kazi ya mtume Paulo na kumalizia mambo ambayo “yalipunguka.” Lakini jambo hili la kuweka wakfu “wazee wa kanisa” halikuwa jambo jipy kwa Wayahudi, kwa maana hata wazee wa sinagogi walikuwa wakiwekwa wakfu.

Mtume Paulo pia alimwandikia Timotheo na kumwambia “Kwa sababu hiyo nakukumbusha, uichochee karama ya Mungu, iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu” (2 Timotheo 1:6). Kuna mifano mingine ya biblia ambayo inaonyesha kwamba sherehe ya kuweka wakfu wachungaji ilikuwa ni wakati wa kutambua uchaguzi wa kiungu ambaao umefanyiwa wachungaji hao wapya na kuwatambua kwa njia ya kuwatenga na kuwatoa kwa ajili ya mwito ambaao wameitiwa na Roho Mtakatifu.

Hata ingawa tukio linalopatikana katika Matendo 13:2-4 halikuwa sherehe kamili ya kuwekwa wakfu, hebu tafakari kuhusu maneno ambayo yanapatikana hapo: “Basi hawa walipokuwa wakimfanya Bwana ibada na kufunga, Roho Mtakatifu akasema, nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia. Ndipo wakiisha kufunga na kuomba, wakaweka mikono yao juu yao, wakawaacha waende zao. Basi watu hao, wakiisha kupelekwa na Roho Mtakatifu ...” Roho Mtakatifu ndiye hutoa vipawa, anawaita wahudumu wa Injili, anawahitimisha na kuwatumu. Lakini pia ni jambo dhahiri kwamba kuna kazi ya kuwatoa wahudumu hao wapya kwa Bwana, na pia kuwaweka muhuri, mambo ambayo ni sehemu ya sherehe ya mchungaji kuwekwa wakfu.

Basi kumweka wakfu mchungaji ni jambo ambalo lina maana zaidi ya mchungaji huyo kupata cheti cha viongozi wa kanisa. Kuna umuhimu mkubwa katika kumweka wakfu mchungaji, kama ambavyo ubatizo wa Mkristo ni jambo lenye umuhimu mkubwa kuliko (tu) tendo la siku moja, tendo la kumtumbukiza Mkristo majini. ■



**“Wahudumu wa Injili,  
ambaao ndio wafanyi  
kazi shambani mwa  
Bwana, wanastahili  
kuwa watu ambaao  
wamechaguliwa na  
Bwana, na kupakwa  
mafuta za nguvu  
na mamlaka yake.”**

Kuweka Wachungaji	Tahariri 3	Viwango vya Kuhitimu	Utaratibu na	Je, Wajua?
Wakfu	Kusudi na Umuhimu	Ambavyo Vimewekwa	Mambo Mengine ya	Usawa wa Huduma
1	wa Kuweka	na Biblia	Kuzingatiwa	
Huduma ya Aina	Wachungaji Wakfu	5		
Moja		Anayewekwa Wakfu		
2	4-5	6	7	9

Kuweka Wachungaji	Tahariri 3	Viwango vya Kuhitimu	Utaratibu na	Je, Wajua?
Wakfu	Kusudi na Umuhimu	Ambavyo Vimewekwa	Mambo Mengine ya	Usawa wa Huduma
1	wa Kuweka	na Biblia	Kuzingatiwa	
Huduma ya Aina	Wachungaji Wakfu	5		
Moja		Anayewekwa Wakfu		
2	4-5	6	7	9

Kuweka Wachungaji	Tahariri 3	Viwango vya Kuhitimu	Utaratibu na	Je, Wajua?
Wakfu	Kusudi na Umuhimu	Ambavyo Vimewekwa	Mambo Mengine ya	Usawa wa Huduma
1	wa Kuweka	na Biblia	Kuzingatiwa	
Huduma ya Aina	Wachungaji Wakfu	5		
Moja		Anayewekwa Wakfu		
2	4-5	6	7	9

Kuweka Wachungaji	Tahariri 3	Viwango vya Kuhitimu	Utaratibu na	Je, Wajua?
Wakfu	Kusudi na Umuhimu	Ambavyo Vimewekwa	Mambo Mengine ya	Usawa wa Huduma
1	wa Kuweka	na Biblia	Kuzingatiwa	
Huduma ya Aina	Wachungaji Wakfu	5		
Moja		Anayewekwa Wakfu		
2	4-5	6	7	9

# MAMBO AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA KUHUSU...

## Neno la Mungu

2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35

## Uhusiano wa Upendo

Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21

## Toba

Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10

## Uzao Mpya

Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4,  
Efe. 2:1, 5-6

## Uhuru Kutokana na Dhambi

1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11

## Ujazo wa Roho Mtakatifu

Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8

## Utakatifu

Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16,  
Tit. 2:11-12, Rum. 6:22

## Ufalme wa Mungu

Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36

## Kanisa

Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13,  
Kol. 1:18

## Umoja

Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4

## Kanuni za Kanisa

Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27,  
Yn. 13:14-17

## Uponyaji wa Kiungu

Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16

## Utakatifu wa Ndoa

Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3,  
I Kor. 7:10-11

## Urembo wa Nje

I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5

## Mwisho wa Nyakati

2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10,  
Mt. 25:31-46

## Kupenda Amani

Lk. 6:27-29, 18:20

## Ibada

Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17

## Wajibu Mkuu

Mk. 16:15

## HUDUMA YA AINA MMOJA

Katika Maandiko tunaona uwekaji wakfu wa wazee, na pia uwekaji wakfu wa mashemasi. Wakati mchungaji anapowekwa wakfu kanisani yeze huwa anawekwa wakfu kama mzee wa kanisa. Katika kanisa la kwanza kulikuwa na vipawa na ofisi tofauti tofauti, na pia kulikuwa na wachungaji wa mahali moja, na wachungaji wa jumla. Wachungaji wa jumla walikuwa wakifanya kazi katika kanisa lote. Basi kulikuwa na utaratibu wa kufuatwa na wahudumu wote wa Injili. Neno mzee wa kanisa ni neno la jumla ambalo linatumika kumaanisha askofu, presbita, msimamizi n.k., na wakati mwingine neno hilo linatumika kwa njia moja au nydinge katika Maandiko. Neno ambalo linatumika katika Tito 1:5 ni "mzee" (*presbuteros*=presbita), halafu andiko hilo linaendelea kuandika kuhusu kuhitimu kwa kiongozi huyo kwa kutumia neno askofu (*episkopos*=msimamizi) kwenye mstari wa saba. Basi presbita na askofu zilikuwa ofisi moja, na ukweli huo ulipotea tu wakati kanisa lilipoanza kuanguka na kuanza kuacha ukweli — jambo ambalo lilitendeka miaka mingi baadaye. Kuhusiana na swala hili mfafanuzi Adam Clarke anasema: "Inaonekana kwamba wale amba waliitwa wazee mahali hapa ni wale pia wanaitwa askofu katika Tito 1:7. Tuna Ushahidi mkubwa kwamba maaskofu na wazee walikuwa watu wenye cheo kimoja katika kanisa la mitume, hata ingawa baadaye ofisi hizo zilifanywa kuwa ofisi tofauti."

Basi kumweka mhudumu wa Injili wakfu ni kumfanya kuwa mzee wa kanisa, na SIO kumaanisha yeze anapewa kazi maalum kanisani mle kama vile mchungaji, mishenari, au mwinjilisti. Mzee aliyewekwa wakfu katika huduma ya unabii ni yule ambaye "ametangazwa kirasmi na kanisa kuwa amehitimu kitabia, kiakili, na kiroho, ya kwamba amehitimu kuchukua mahali pa mchungaji pale kanisani" (*The Apostolic Church/Kanisa la Mitume*, Charles E. Brown, 1947 uku. 151).

Lakini wakati kanisa lilipoanza kupotoka na baadaye likafanya kuwa kanisa la Ukatoliki wa Kirumi, nguvu za wachungaji zilianza kukua sana kanisani, na wanadamu wakaja kuchukua wajibu amba Roho Mtakatifu alitaka kutimiza katika maisha ya kanisa. Na jinsi karne zilivyo zidi kuendelea ndivyo vyeo tofauti tofauti vilizidi kuundwa kanisani kwenye sehemu tofauti za uongozi, vyeo ambavyo havikuwako katika kanisa la mitume.

Maandiko yanatufundisha kwamba serikali ya kanisa imo mikononi mwa Yesu, lakini pia yanatufundisha kuna uongozi wa wanadamu humu kanisani kuititia kwa Roho Mtakatifu ambaye ndiye hutoa vipawa vyake kwa wanadamu. Ni jambo la lazima kwa kila mhudumu wa injili ambaye anadai kwamba anafanya kazi ya injili kutokana na kupata kipawa na Roho Mtakatifu, wakati akifanyisha kazi kipawa hicho chake, anastahili kuruwahuwu wachungaji wale wengine amba pia wamejazwa Roho Mtakatifu, kukagua ukweli huo ulio ndani yake: "Na roho za manabii huwatii manabii" (1 Wakorintho 14:32). Lakini jambo hili halitimii kwa njia ya mchungaji huyu mpya kukaguliwa na wachungaji wengine waliowekwa wakfu na amba wana vyeo tofauti na vyenye nguvu kanisani, bali ni kwa watu wa Mungu wanaongozwa na Roho Mtakatifu kufanya kazi kwa unyenyekevu na umoja. ■

Gazeti la *Ukweli wa Injili* ni jalida ambalo linatolewa kila robo ya mwaka kwa manufaa ya Kanisa la Mungu kwa ajili ya mafundisho na kwa ajili ya kuwashimiza Wakristo ili washike kweli za Biblia. Tutembelee katika tovuti yetu ya [www.thegospeltruth.org](http://www.thegospeltruth.org) na ujiandikishe ili uwe ukitumiwa notisi kwa njia ya barua pepe kila wakati jalida hili likiwa tayari ili uweze kupata toleo la kila kipindi. Gazeti hili la *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika nchi nyingi ili lisambazwe katika nchi hizo. Kazi hii inawezekana kuititia kwa matoleo yanayotolewa kwa hiari. Pia wewe ukitaka unaweza kutumiwa risiti ya vile tumelipa ushuru kutokana na zawadi yako.

—Mhariri, Michael Smith

Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA  
editor@the gospeltruth.org

# Tahariri



*Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri? Tena wahubirije, wasipopelekwa? Kama ilivyoadikwa, Ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema! — Warumi 10:14-15*

Mimi nina furaha nyingi moyoni mwangu kwa ajili ya wale ambao wameitwa na Mungu na ambao wanahubiri injili ya Yesu Kristo kwa uaminifu. Roho Mtakatifu ndiye huita watu katika huduma kupitia kwa uwezo wake wa kiungu. Somo la muhula huu linahusiana na kuwekwa wakfu kwa wachungaji. Bwana akipenda tutashughulikia kuwekwa wakfu kwa mashemasi katika jalida litakalofuata. Walakini neno "kuwekwa wakfu" haliwfurahishi watu wengine kwa sababu hili ni jambo ambalo wakati mwingine limetumiwa kwa njia ambayo haifai, likakosa kueleweka, likafanya watu wengine kuumia miyoni, na hata kuweza kutumiwa vibaya na viongozi wa kanisa. Ombi langu ni kwamba kulingana na jinsi ambavyo watu watazidi kuelewa swala la kuweka wakfu wachungaji, jambo hili litakuja kuchukuliwa kuwa la kupendeza kanisani.

Kuwekwa wakfu kwa wachungaji ni jambo ambalo ni zaidi ya mtu kupewa kijikaratasi kwa ajili ya kutimiza sheria. Sherehe ya kuweka wakfu hufanyika kama ushuhuda na dhibitisho kwa kanisa kuhusu wito wa Roho Mtakatifu na upako wake katika maisha ya mchungaji huyo anayewekwa wakfu. Mfano wa mwanzo wa jambo hili na mafundisho kuhusiana na swala hili ni mambo ambayo yanapatikana katika Neno la Mungu, ndiposa swala hili ni zaidi ya maoni au mawazo ya watu binafsi. Kumweka mchungaji wakfu ni tendo la kiroho la kumtoa mtu kwa Mungu, yeye pia anapata nafasi ya kujitao kwa Mungu, na pia ni wakati wake kupata baraka maalum na wema wa Roho Mtakatifu kupitia kuwekewa mikono na wachungaji wale wengine.

Kama jinsi ilivyo kwa mafundisho na mazoea mengine ya mambo ya biblia, ni jambo muhimu sisi kuelewa swala hili kwa kiwango ambacho kinakubaliana na mambo yale mengine ya kiroho. Ukweli ni kwamba, kuwekwa wakfu kwa mchungaji hakustahili kuchukuliwa kuwa ni yeye kupewa cheo cha kujionea fahari. Mle kanisani hakustahili kuwa na vyeo na viwango tofauti tofauti, kama ambavyo inaonekana katika vikundi vingine vya kidini. Wahudumu wote wa injili wanatumika katika cheo kimoja, na wote wanastahili kupata upako wa Roho kwa ajili ya huduma wanayofanya, iwe ni wale waliowekwa wakfu au hata wale ambao hawajawekwa wakfu. Lakini pia ni kweli kwamba kuwekwa wakfu ni jambo lenye maana, ndiposa kuna wakati ambapo wachungaji waliowekwa wakfu huwa na mamlaka ya Mungu na ya mwanadamu ambayo mtumishi ambaye hajawekwa wakfu anaweza kukosa. Mchungaji aliyewekwa wakfu ANASTAHILI kuwa kwamba amehitim, na pia awe amepakwa mafuta na Bwana bila kuwa na kizuizi chocote kile, na hata watu anaowahudumia wanastahili kuwa na imani naye.

Ni jambo muhimu kwamba kuwekwa wakfu kwa wachungaji liwe jambo linaloshughulikiwa kwa njia inayolingana na Maandiko. Tendo hili la kumweka wakfu mchungaji linaweza kupoteza umuhimu wake wa kiroho katika mwili wa Kristo ikiwa watu ambao hawastahili, na ambao ni wapya katika ukweli watawekwa wakfu kuwa wahudumu wa injili kwa kusudi la kumpendeza mchungaji fulani, au kulipendeza kanisa. Hili jambo huwa ni tatizo katika nchi nyingi. Kuwekwa wakfu wachungaji haistahili kuwa ni silaha ya kisiasa ya kumpendeza mtu yejote. Basi ni ombi langu kwamba Mungu atasaidia Kanisa la Mungu ili lidumishe usafi wa mafundisho yanayohusiana na kuwekwa wakfu kwa wachungaji.

Kwa njia ya nyongeza tungependa kusema kwamba kuna maandiko katika Agano Jipyambayo yanatumia neno 'kuweka' wakfu (tazama Matendo 1:22; 1 Timotheo 2:7; Matendo 14:23) kwa njia ambayo haizungumzii tendo la kuweka wakfu wachungaji, ambalo ndilo jambo linalozungumziwa na maandiko mengine. Katika jalida hili mimi nitashughulikia maandiko yale tu ambayo yananena kuhusu sherehe za kuweka wakfu wachungaji. Hebu kila mmoja wetu tuishi kwa njia ambayo inamtukuza na kumpendeza Mungu. Kwa sababu kulingana na maneno ya Ndugu Ostis Wilson, "Tukimpendeza Mungu pia tutampendeza yejote yule ambaye anastahili kupendezwa."

Michael W. Smith

Julai 2020

## Changa Moto

[Ndugu Ostis Wilson, akisema kuhusu Matendo 13:1-4, mahali ambapo mitume Baranaba na Sauli wanawekwa wakfu kwa ajili ya kazi ya Bwana]

"Haya yalikuwa maagizo mtakatifu na yenyewe uzito mkubwa, ndiposa watu hawa wakafunga na kuomba kabla ya kufanya hivyo, na tena wakafanya vivyo hivyo hata baada ya Roho Mtakatifu kunena nao. Wao walitaka kuwa na uhakika kwamba hawakuwa wamepotea njia. Enyi ndugu zangu, hebu tupate onyo kidogo hapa kuhusiana na jambo hili na tuweze kuchukulia ibada zetu za kuweka wakfu wachungaji kuwa ni wajibu mzito zaidi na wenye kuhitaji utakatifu zaidi ya jinsi ambavyo tunachukulia (wakati mwingine) kwa sasa. Mimi mwenyewe ninajihisi kwamba ninaweza kufanya hivyo."

# WACHUNGAJI WAKFU

**Kuna sababu nyingi muhimu za kuweka wakfu wachungaji katika Kanisa la Mungu. Hizi sababu zinahitaji kuchukuliwa kwa umuhimu wake, bila kulemazwa kwa njia ya watu kufuata malengo ya kibinaksi, falsafa duni, au mapendeleo kwenye shughuli hii muhimu ya kanisa.**



## Kuweka Uhakika kwa Jambo Ambalo ni la Kiroho

Kulingana na maandiko kuna jambo la kiroho ambalo hupatikana wakati mchungaji anapowekwa wakfu na wachungaji wale wengine. Mtume Paulo alikuwa akisema kuhusu jambo hili wakati alipompatia Timotheo maagizo yafuatayo:

*"Usiache kuitumia karama ile iliyomo ndani yako"* (1 Timotheo 4:14). Mtu akichunguza andiko hili atapata ukweli mwingsi kuhusiana na swala la kuweka wakfu wachungaji.

*Usiache kuitumia karama ile iliyomo ndani yako:* Neno "karama" hapa limetafsiriwa kutoka kwa neno la Kiyunani karisma (*char'-is-mah*)—ambalo lina maana ya kupata wema wa kiungu, kupewa kipawa cha kiroho, kuhitimu kwa mambo ya dini, ya watu ambaao anahudumia.

na kupata fadhili. Ukamilifu wa huduma ya Timotheo – wito wake, kuhitimu kwake, ofisi ambayo alikuwa asimamie, kipawa cha Mungu kilichokuwa ndani yake, na kuwekewa wakfu kwake, yote yalikuwa sehemu ya wema wa Mungu ambaao Timotheo aliagizwa asiache. Mtume Paulo alinena tena kuhusu karama hiyo katika 2 Timotheo 1:6 "Kwa sababu hiyo nakukumbusha, uichochee karama ya Mungu, iliyo ndani yako kwa kuwekewa mikono yangu." Mtume Paulo alikuwa akinena hapa kama ambavyo baba ya mtoto huzungumza na mtoto wake, "Kuwa mwaminifu kwa karama na agizo ambalo umekabidhiwa." Huduma ya Timotheo, wito wake, na kuhitimu kwake — yote yalikuwa mambo ambayo yalitokana na kipawa cha Mungu. Ndugu zake kanisani ambaao walitambua wito aliokuwa nao Timotheo na kuhitimu kwake ndio walihitimisha kipawa hicho na kikitambua kwa njia ya kumwekea mikono wakati alipowekwa wakfu. Ndiposa tunasema kwamba kuwekewa wakfu huku kulikuwa ni "sehemu" ya kipawa (karama) au mapato ambayo Timotheo alikuwa ashapokea.

**Kuwekewa mikono:** Kwa kiwango fulani kipawa cha huduma kilitolewa na Roho Matkatifu kuitia kwa tendo la kuwekewa mikono, kama ilivyo dhahiri kwa njia ya mtume Paulo na wazee wa kanisa. Kuna mengi ambayo tunasoma kutoka kwa Biblia kuhusiana na uwekelewaji mikono. Katika Mwanzo 48:14 Israeli aliwawekea

Efuraimu na Manase mikono na kuwabariki. Katika Hesabu 27:18-20 Bwana alimwagiza Musa kumwekea Yoshua mikono mbele ya kuhani na umati wa wana wa Israeli. Musa pia alikuwa ayatoe maagizo kwa Yoshua na kumpatia Yoshua heshima yake mwenyewe ili wana wa Israeli waweze kumtii Yoshua. Kumbukumbu la Torati 34:9 ni andiko ambalo linaweka muhuri umuhimu wa tendo hilo: "Na Yoshua, mwana wa Nuni, alikuwa ameja roho ya hekima; maana Musa alikuwa amemwekea mikono yake juu yake; wana wa Israeli wakamsikiliza, wakafanya kama BWANA alivyomwamuru Musa." Ni jambo la kuzingatiwa kwamba, wakati mwingsi katika Kanisa la Mwanzo Roho Mtakatifu alitolewa kwa waumini wapya kwa njia ya wao kuwekewa mikono na kuombewa. Roho Mtakatifu alipenwa na Mungu, lakini pia kulikuwa na nguvu na kipawa maalum ambacho kilipatikana kuitia kwa maombi ya pamoja yaliyofanywa kwa yule ambaye ni mtoaji wa vipawa. Kuna nguvu nyingi zinazopatikana kwa njia ya maombi ya kukubaliana na fadhili zake Mungu, mambo ambayo chimbuko lake kwa sehemu fulani ni mtu kuwekewa mikono. Jambo hili linaenda sambamba na "kumwekea mikono" mchungaji kwa kusudi la kumwekea wakfu kwa ajili ya huduma ya uchungaji.

**Ya wazee.** Chimbuko la neno hili *wazee* ni neno *presbiteri* ambalo ndilo linapatikana katika Luka 22:6 na Matendo 22:5. Kuwekewa wakfu ni tendo ambalo halikufanywa na mchungaji mmoja tu bali lilifanywa na kamati au kundi la wazee.

## Kutambuliwa Hadharani kwa Wito wa Kiroho

Mchungaji kuwekewa wakfu ni njia moja kati ya nyingi za kuweka muhuri huduma ya mchungaji huyo kati ya watu ambaao anahudumia. Hii ni njia ya kutambua kile ambacho Mungu anafanya katika maisha ya mtu fulani na ni njia moja ya kusaidia mhudumu wa injili kukubalika kwa watu na kwa mwili au huduma fulani ya Wakristo. Wakati ambapo mchungaji aliyewekwa wakfu anaposhughulikia maswala ya wale anaohudumia, ye ye anahitaji kuhisi kwamba anaungwa mkono na kusaidiwa na huduma ya kanisa lote ambako anahudumu. Ni jambo muhimu watu kujua na kuelewa kwamba mchungaji ambaye amewekwa wakfu anawakilisha kitu kikubwa zaidi ya ye ye binaksi—kwamba anawakilisha mwili wa Kristo. Hii ni sababu moja ya *kwa nini tunahitaji kushughulikia* swala hili la kuweka wakfu kwa umakini mkubwa.

Ndugu Ostis Wilson aliandika mambo yafuatayo kuhusiana na swala hili: "Nina uhakika kwamba tendo

(Endelea katika Ukurasa 5)

(Inaendelea kutoka Ukurasa 4)

la kumtambua mchungaji hadharani ni njia kubwa ya ye ye kuijishi kwamba anaungwa mkono na wachungaji ambao atakuwa akifanya kazi nao, na katikati mwao; lakini mimi najihisi kwamba ibada ya kumweka wakfu mchungaji ni jambo kubwa hata zaidi ya hivyo, kwamba tendo la mhudumu kuwekewa mikono na watu ambao wamejazwa Roho Mtakatifu ni tendo ambalo litamtunukia mtu huyo kipawa fulani . . . mtume Paulo amelihakiki jambo hilo . . . ya kwamba kuna kitu ambacho mtu hupata kupitia kwa kuwekewa mikono na wachungaji ambao wamejazwa Roho Mtakatifu. Mimi najihisi kwamba tunahitaji kufundisha watu wetu jambo hili, na hasa kuwafundisha wale ambao wanataka kuwekewa wakfu kwa kusudi la kuwaandaa ili kutarajia kipawa maalum [baraka/wema/kuwekewa muhuri—*mhariri*] kutoka kwa Mungu, wakati ambapo watawekelewa mikono na wachungaji ambao tayari wamejazwa Roho Mtakatifu.”

### Serikali ya Kanisa


Tito 1:5 ambayo imenukuliwa hapo mbeleni inasema: “Ili uyatengeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru.” Maandiko ambayo yanafuata andiko hili hapo katika kitabu cha Tito yanaeleza viwango vya kuhitimu ambavyo vililitajika kwa wazee ambao walikuwa wawekwe wakfu. Katika andiko hili kuwekewa wakfu huku kunapewa umuhimu mkubwa. Sababu moja ya kuweka wakfu wazee ni ili kuwe na uongozi ambao unatambuliwa na pia mamlaka ya kiroho humo kanisani. Kulikuwako (na daima kutakuwa) na roho pingamizi katika kazi ya Bwana, na kuwekewa wakfu kwa viongozi wachungaji ambao wamejazwa Roho Mtakatifu na ambao wanatambuliwa ni jambo ambalo linaweza kuweka wazi na kufanya kuwe na maongozi bora wakati misukosuko inapokuja. Basi wazee kuwekewa wakfu ni jambo ambalo lilianzisha maongozi bora katika serikali ya kanisa na ambayo imewekwa madarakani na Roho Mtakaifu. Wakati kuna sauti tofauti tofauti, ni jambo la msaada mkubwa watu kujuua kwamba kuna kiongozi wa kiroho ambaye anatambuliwa na ambaye aweza kuaminwi ili kutoa miongozo kwao kwa njia inayolingana na utakatifu. Hebu tukumbuke maneno ambayo yaliandikwa na viongozi wa Kanisa la Mungu katika siku zilizopita kuhusiana na swala hili:

“Ni wazi kwamba makanisa ya kwanza ‘yaliongozwa’ na mitume hapo katika siku za mwanzo, lakini ‘uongozi’ huu haukuwa rasmi. Uongozi wenywewe ulionekana kwa jinsi Wakristo wa wakati huo walivyoahidiwa na kuongozwa na tabia nzuri na za kiungu pamoja na maadili ya hali ya juu ya viongozi hao ambao waliheshimiwa na kuaminika sana; jambo ambalo pia limeonekana kwa kufuata utaratibu huo katika vizazi vingine vyote vya kanisa, hata ingawa sio kwa kiwango hicho (hicho) ambacho kilidhihirishwa na viongozi wa kanisa la kwanza.” *The Apostolic Church – (Kanisa la Mitume)*, Charles E. Brown, 1947, uku. 123).

“Kwa kweli kuna serikali katika Kanisa la Mungu, serikali ambayo ni ya wanadamu—wanadamu ambao wamepewa karama na Mungu, wakifanya kazi pamoja na viongozi wale wengine ambao wamepewa karama na Mungu, huku wakiwa chini ya uongozi wa Roho

Mtakatifu.” *Church of God Doctrines (Mafundisho ya Dini ya Kanisa la Mungu)*, Cecil Carver, 1979, uku. 95.

“Ni dhahiri kwamba mchungaji ye yote yule atajishi kuwa huru zaidi katika kufanya kazi yake ya huduma wakati akijua kwamba ametambuliwa na kuungwa mkono, na hata kwamba washirika na wachungaji wale wengine wamesimama naye na wanamkulabi. Ili mtu aweze kufaulu kutimiza wajibu wote wa “Mzee” au “Askofu” katika kanisa fulani ye ye anahitaji kuwekewa wakafu kwa njia ya kuwekewa mikono na wachungaji wengine ambao tayari washawekwa wakfu. Inawezekana kuwe ni kweli kwamba mhudumu huyo ana uwezo wa kuhubiri na kulisha kundi la Bwana kabla ya ye ye kuwekewa wakfu, lakini inapofika swala la kutumia mamlaka, na pia kwa kushughulikia shida ambazo zaweza ibuka katika kusanyiko la kanisa, ye ye atafaulu zaidi na kuheshimika katika maamuzi yake ikiwa atatambuliwa na kuungwa mkono na kanisa ambalo anatumika ndani mwake pamoja na watu ambao anahudumia.” *Faith and Victory* (Imani na Ushindi), Ostis Wilson, Disemba 1979.



Wakati kuna sauti tofauti tofauti, ni jambo la msaada mkubwa watu kujuua kwamba kuna kiongozi wa kiroho ambaye anatambuliwa na ambaye aweza kuaminwi ili kutoa miongozo kwao kwa njia inayolingana na utakatifu.

### Mambo ya Sheria

Kirasmi na kisheria kumweka wakfu mchungaji ni kusema kwamba mtu huyo sasa ametambuliwa na kukubaliwa kama mchungaji katika ushirika fulani au kanisa fulani. Hili ni jambo ambalo linatakikan na serikali kadha wa kadha, na hata vikundi kadha wa kadha, ili wahudumu wa injili waruhusiwe kufanya shughuli fulani za wachungaji (kama vile kushikanisha ndoa, kufanya huduma magerezani, na hata kuwatemebelea wagonjwa waliomo katika manyumba ya wagonjwa wasiojiweza, wanaosubiri siku yao ya mauti, n.k.).

### Kukubalika Kibinafsi

Huduma ina upweke mwingi, iwe kwamba mchungaji amewekwa wakfu au la, lakini kuna nguvu na faraja ambazo mchungaji hupata kwa kujuua kwamba wahudumu wenzake wanamuunga mkono na wanatambua uongozi na upako wa Mungu maishani mwake. Ni kweli kwamba hii sio sababu nzuri ya kumweka wakfu mchungaji, lakini kuna umuhimu wa jambo hili, kwa maana ni jambo ambalo linaweza kukatisha makali ya maswali ambayo yanatoka ndani na nje ya kanisa, wakati ambapo mambo mengine yote yako shwari maishani na katika huduma ya mchungaji huyo mpya. ■

# YULE ANAYEWEKWA WAKFU

## Matakwa ya kuwekwa wakfu



**"Mhudumu wa injili anastahili kuwa mwakilishi wa mwili wa Kristo na kuwa mfano bora wa maisha ya utakatifu, mtu mwenye msimamo timamu kuhusiana na mafunzo ya kidini, na roho yake kuwa ya mfano wa Kristo."**

**Kuhitimu kwake:** Mtu ambaye anataka kuwekwa wakfu kama mchungaji anahitaji kuwa na upako na wito wa Mungu kwa ajili ya huduma, na pia anahitaji kuwa amefuzu kwa viwango fulani vinavyotakikana kwa askofu wa kanisa kama ilivyoandikwa katika 1 Timotheo 3:1-7. Viwango hivyo vya kuhitimu vinahitajika kwa wahudumu wote wa Injili; lakini bila shaka vinahitajika kuwa dhahiri kabisa katika maisha ya mchungaji kabla ya yeye kuwekwa wakfu. Mhudumu wa injili anastahili kuwa mwakilishi wa mwili wa Kristo na kuwa mfano bora wa maisha ya utakatifu, mtu mwenye msimamo timamu kuhusiana na mafunzo ya kidini, na roho yake kuwa ya mfano wa Kristo. Kwa jumla upako wa Roho Mtakatifu ulio ndani yake unahitaji kuwa dhahiri kwa mwili wa Kristo, na sio tu kwa watu wachache. Wanafunzi wanaowekwa wakfu wanahitaji kuwa na mazao ya huduma, mazao yanayoweza kuonekana, na pia wanahitaji kuwa watu walio wa msaada kwa huduma ya kanisa, wasiwe watu wa kuleta hasara. Wanahitaji kuwa watu wanaoshughulikia mambo yao kwa uadilifu, iwe ni mambo ya ulimwengu huu au ya kiroho, na pia wanastahili kuwa watu wanaoweza kuaminika na washirika wa kanisa. Hata ingawa kuwekwa wakfu kwa mchungaji ni wito mkuu maishani mwake, hatustahili kufikiria kwamba hii ni kusema kwamba mtu huyo ni mkamilifu, kwa maana kila mmoja wetu hufanya makosa wakati mmoja au mwengine, sisi sote tuna udhaifu, na kila mmoja wetu ana sifa za kuzaliwa nazo ambazo Mungu angali anashughulikia ili kuturekebisha.

**Vizuizi vya kuwekwa wakfu:** Kando na viwango vya kuhitimu ambavyo tayari tushavitaja, yafuatayo ni baadhi ya mambo ambayo yanaweza kusitisha mhudumu wa injili kuwekwa wakfu: ikiwa maisha yake ya kinyumbani si mazuri, ikiwa maishani mwake kumeonekana mfuatano wa matatizo, ikiwa washirika wa kanisa hawana na imani naye, ikiwa mtu hajawa mwaminifu katika huduma, na ikiwa ni mtu asiye na hekima katika mahubiri yake na jinsi anavyohubiri, na ikiwa yeye ni mtu ambaye hana umoja na sehemu ile nyininge ya mwili wa Kristo, n.k.

**Wakati unaofaa:** Mchungaji ambaye ni mpya katika huduma hastahili kuwekwa wakfu hata kama yeye yuko na miaka mingi na ufahamu mkubwa. Mtu kama huyo anastahili kupewa

muda wa kudhihirisha huduma yake ndani ya Bwana, kwa maana kuna mitego ya kiroho ambayo amewekewa na adui. Ndugu Cecil Carver alisema yafuatayo, "Neno la Mungu linatufunza kwamba mhudumu wa injili hastahili kuwekwa wakfu hadi adhihirishe kwamba yeye anastahili kuwekwa wakfu. 'Asiwe mtu aliyeongoka karibu' ni jambo linaloonyesha kwamba viongozi wanahitaji kuwa waaangalifu kabla ya kumweka mtu wakfu. Lakini kwa upande mwengine viongozi wa kanisa hawastahili kuchelewesha mhudumu wa injili kuwekwa wakfu kwa muda mrefu sana." *Church of God Doctrines (Mafundisho ya Dini ya Kanisa la Mungu)*, 1979

Kuweka wakfu mchungaji silo jambo la kuchukuliwa kwa urahisi, bali ni jambo linalostahili kuchukuliwa kwa uangalifu wa kiungu. Mtume Paulo alitoa agizo katika 1 Timotheo 5:22 "Usimwekee mtu mikono kwa haraka, wala usizishiriki dhambi za watu wengine." Kama kiongozi wa kanisa atamweka wakfu mchungaji ambaye hastahili, basi yeye atakuwa ni mshiriki wa kutostahili huko kwake, kwa sababu yeye ndiye aliyemhitimisha mhudumu huyo mpya. Zaidi ya hayo mchungaji ambaye tayari amewekwa wakfu hastahili kukubali msukumo wa kumweka wakfu mtu mwengine kama Roho Mtakatifu hajampatia yeye uwazi na uhakika kuhusiana na swala hilo. Kumweka mtu wakfu ili kumhitimisha kwa taratibu za kiserikali (kama vile kufunga ndoa n.k.) si jambo linalokubaliana na umuhimu wa sherehe hii ya kuweka wakfu wachungaji, isipokuwa iwe kwamba mchungaji huyo amehitimu katika viwango vingine vyote vinavyotakikana.

Jambo hili pia ni kweli ikiwa mhudumu huyo wa injili ametoka katika dhehebu nydingine, au kanisa lingine. Hata ingawa inaonekana mtu huyo ana upako wa Mungu, na kwamba anakubali ukweli wa injili, kupita kwa wakati ndilo jambo lenye uhakika la kuonyesha kwamba mtu huyo anao mwito wa kuhubiri injili katika maisha yake.

1 Wathesalonike 5:12 inasema, "Lakini, ndugu, tunataka mwatambue wale wanaojitaabisha kwa ajili yenu." Kujuja yale mambo ambayo mtu anaamini, na pia kujuja maisha yake, ni jambo ambalo huchukua muda, ndiposha si jambo la busara kumweka wakfu mchungaji ambaye anataka tu kujulikana kwa haraka katika Kanisa la Mungu.

(Endelea katika Ukurasa 7)

(Inaendelea kutoka Ukurasa 6)

**Mambo mengine ya kuzingatia:** Maandiko hayajasema mtu anastahili kuwa mchungaji kwa muda gani kabla ya yeze kuwekwa wakfu, basi muda huo utakuwa tofauti kutoka kanisa moja hadi lingine. Ndugu Ed Wilson, ambaye ni mzee wa kanisa katika Kanisa la Mungu, alisema jambo ambalo tunastahili kutafakari juu yake kuhusiana na swala hili. Ikiwa mtu amekuwa akifanya huduma madhabahuni toka muda wa miaka tano hadi saba, huenda ikawa huu ni wakati bora wa kuwe na mjadala ikiwa atawekwa wakfu au la. Huu ni wakati bora wa aidha kumweka wakfu au kumpatia sababu za kutomweka wakfu. Basi ikiwa mtu amekuwa katika huduma kwa miaka mingi na bado hajawekwa wakfu litakuwa jambo bora kwake kuuliza kwa unyenyekevu kama kuna kizuizi chochote cha yeze kuwekwa wakfu.

Kama mhudumu wa injili ana upungufu maishani mwake anahitaji kuendelea kuomba, huku akimtafuta Mungu, na kufanya kazi ndani yake Roho Mtakatifu. Pia anahitaji kufanya kazi katika kanisa lake ili aweze kutimiza kwa neno na kwa matendo kile ambacho kimekuwa kipungufu maishani yake. Ni jambo ngumu mtu kukubali kuachana na huduma ya kuhubiri injili, lakini ikiwa upako na wito wa Mungu haupo, au ikiwa hautambuliwa na wachungaji wengine waliojazwa Roho Mtakatifu, kuna wakati ambako mtu anastahili kuachana na kazi hiyo kwa ajili ya kuinuifaisha injili, na kwa sababu ya manufaa ya washirika wale wengine wa kanisa. Kuwekwa wakfu si jambo la kukazania kwa nguvu, na pia si jambo la kujivunia, na hata sio kipimo cha kufaulu au kutofaulu kwa mtu. Mhudumu wa injili hana haja ya kukazana ili awekwe wakfu kwa sababu "Zawadi ya mtu humpatia nafasi . . ." (Mithali 18:16). ■

## Viwango vya Kuhitimu kwa Askofu Ambavyo Vimewekwa na Biblia

1 Timotheo 3:1-7

Ni neno la kuaminipa; mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema.

Basi imempasa askofu awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji, ajuaye kufundisha;

si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga watu; bali awe mpole; si mtu wa kujadiliana, wala asiwe mwenye kupenda fedha; mwenye kuisimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu;

(yaani, mtu asijejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje Kanisa la Mungu?)

Wala asiwe mtu aliyeongoka karibu, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi.

Tena imempasa kushuhudiwa mema na watu na watu walio nje; ili asianguke katika lawama na mtego wa Ibilisi.

## Utaratibu Unaofaa Na Mambo Mengine MUHIMU KATIKA IBADA YA KUWEKA WAKFU



Biblia haijatupatia mpango kamili wa jinsi ya kuendesha ibada ya kuweka wakfu. Kile ambacho biblia imetupatia ni viwango vya kuhitimu ambavyo vinahitajika kwa wale wanaowekwa wakfu, halafu ikaacha mambo mengine mikononi mwa viongozi wa kiungu ambaao wanaongozwa na Roho Mtakatifu. Basi taratibu ambazo tutajadili hapa si miongozo kutoka kwa biblia ambayo ni lazima kufuatwa na kila mchungaji, ila ni mambo tu ya kuzingatia ili kazi hiyo ya kuweka wakfu wachungaji ipate ifaulu na iwe yenye manufaa. Kama alivyofanya mtume Paulo mimi nawaandikia mambo hayo kwa kutumia kibali tu, bali sio kama amri ambayo ni ya lazima kufuatwa.

**Wajibu:** Wajibu wa kumweka wakfu mhudumu wa injili ni wa mchungaji na viongozi wengine wa kiroho ambaao wanajua maisha ya mhudumu huyu (vizuri). Yule ambaye ataongoza sherehe ya kumweka wakfu anastahili kuwasiliana na wazee wengine ambaao wamefanya kazi na mhudumu huyo mpya ili aweze kujua kama viongozi wale wengine wako na mzigo na jambo hilo, na kama wao wanamuunga mkono. Kuna wakati ambapo mhudumu wa injili amekosa kuwekwa wakfu kwa sababu hakuna mtu ambaye amechukua jukumu hilo kutokana na umbali wa mahali ambapo mhudumu huyo mpya anahudumu n.k. Basi sababu kama hiyo haistahili kuchukuliwa kuwa ni upungufu ambaao uko ndani ya mhudumu huyo mpya ambaye bado hajawekwa wakfu.

Wachungaji hawastahili kukubali kusukumwa kumweka wakfu mtu fulani wakati ambapo hawana utimamu na pia "faraja ya kiroho" kuhusiana na mtu huyo ambaye anataka kuwekwa wakfu. Ni jambo rahisi "zaidi" kanisa

(Endelea katika Ukurasa 8)

**"Mhudumu wa injili anastahili kuwa mwakilishi wa mwili wa Kristo na kuwa mfano bora wa maisha ya utakatifu, mtu mwenye msimamo timamu kuhusiana na mafunzo ya kidini, na roho yake kuwa ya mfano wa Kristo."**

(Inaendelea kutoka Ukurasa 7)

kushughulikia swala maalum, kuliko wakati ambapo kuna hali ya kutotosheleka kanisani mwote kuhusiana na swala hilo. Kujipatia muda ni jambo ambalo limekuwa la hekima na manufaa makubwa hapo mbeleni, ikiwa kungali kuna hali ya kutosheleka kuhusiana na mhudumu huyo anayetaka kuwekwa wakfu. Kuwekwa wakfu ni jambo la kiroho, na pia ni jambo ambalo halihitaji msukumo na siasa au kufanywa ili kumfurahisha mtu fulani. Zaidi ya hayo, kuna jukumu ambalo wale wanaomweka mhudumu huyo mpya wakfu wanao kuhusiana na maisha yake.

**Kukagua maisha ya anayewekwa wakfu:** Kumuuliza maswali ya ukaguzi mhudumu ambaye anayekwa wakfu ni jambo la busara. Yule mchungaji ambaye anamweka wakfu mhudumu huyu mpya anahitaji kuzungumza naye kuhusiana na maswala na mafundisho ya dini ili kuhakikisha kwamba yeze anaewela (mambo) yote. Pia ni jambo bora kutembelea mke au mume wa mhudumu huyo mpya ili kuhakikisha kwamba hali ya kiroho ya familia yake iko sawa, na kwamba watu wake wana imani naye. Wachungaji wanaomweka wakfu mhudumu huyo mpya wanahitaji kutangaza jambo hilo kanisani, mahali ambako anahudumu. Wakati mwagine kunaweza kuwa na shida zilizojificha na ambazo zinaweza kuibuka ikiwa hatua hizi zitafuatwa. Ni vyema zaidi kushughulikia shida hizo kabla ya mtu huyo kuwekwa wakfu badala ya kufanya makosa ambayo hayawazi kufutika.

Kuwekwa wakfu ni jambo ambalo linahusu uhusiano wa pande zote mbili. Sio tu kwamba huduma au kanisa letu linamuunga mkono na kutangaza kwamba liko nyuma ya mchungaji huyo mpya, bali pia anayewekwa wakfu anatangaza kwamba amekubali Kanisa la Mungu na yale yote ambayo kanisa hilo linafundisha

kama mwili wa Kristo. Kuwekwa wakfu ambako kunaweza kufanyika na kikundi kilichojitenga kanisani ni jambo ambalo halitakuwa na maana yoyote na ambalo halitambuliwi kamwe na Kanisa la Mungu.

Sherehe hii ya kuweka mchungaji wakfu si jambo linalolenga kumwingilia mtu maishani yake ya kibinagsi, lakini pia ni jambo ambalo linahitaji kufanywa kwa kumakinika sana. Kumkagua anayewekwa wakfu halistahili kuchukuliwa kuwa ni tendo la kumhukumu mhudumu huyo mpya, bali ni njia ya kuleta uhakika kwa mambo yote. Wale ambao wanataka kuwekwa wakfu hawastahili kuogopa au kupinga utaratibu huu. Uwekaji wakfu ni jambo ambalo linastahili kuleta baraka ya Mungu kwa mwili wote wa Kristo.

**Uwazi:** Ni jambo la heshima mchungaji kupasha habari wachungaji wengine katika mwili wa Kristo kuhusiana na swala hilo la kumweka wakfu mhudumu huyo mpya wa Injili. Hata ingawa wazee wawili au watatu wanaweza kuwa na kibali kinacholingana na biblia cha kumweka wakfu mtu fulani, hali halisi ya kazi ya uwekaji wakfu inahusisha haja ya kanisa lote na huduma yote kuwa na uhakika na kuunga mkono jambo hilo. Kuweka wakfu ambako kutafanyika kwa siri au kwa kutokuwa na uwazi ni jambo ambalo litalemaza moja ya kusudi kuu la kufanyika kwa sherehe hiyo. Basi hili ni jambo ambalo linahitaji kuendeshwa kwa njia inayoleta sifa kwa sherehe hizo.

**Mahali:** Ni baraka kwa watu wa Mungu na pia ni ushuhuda kwa kazi ya Roho Mtakatifu ikiwa ibada ya uwekaji wakfu itafanywa mbele ya mwili wa waumini. Pia ni jambo bora kwa mchungaji kuwekwa wakfu mbele ya watu wale ambao yeze anahudumia. Kuweka wakfu ni kutambua kwa njia rahisi na kufurahia kile ambacho Mungu anafanya ndani ya maisha ya mhudumu wa injili na kupitia kwa maisha yake. ■

Kuweka wachungaji wakfu ni jambo ambalo limefundishwa katika Biblia, na pia ni jambo ambalo ni muhimu katika maendeleo ya kanisa la Mungu, hata katika siku hizi zetu. Basi hili ni jambo ambalo linastahili kuchukuliwa kwa umuhimu wake na kupewa heshima zake. Wazee ambao tayari wamwekwa wakfu wanastahili kupata heshima zao kutokana na kazi yao, na kutokana na mamlaka walio nayo ndani yake Roho Mtakatifu.

Mtume Paulo aliandika katika 1 Timotheo 2:7 na kusema, "Nami kwa ajili ya huo naliwekwa niwe mhubiri na mtume . . ." Baadhi ya wachambuzi wametafsiri neno hilo "kuwekwa" (wakfu) kwamba sio sherehe ya kutambua huduma ya mhudumu wa injili kwa njia hiyo ya kuwekewa mikono, bali ni wito wa kiungu ambao ulikuwa maishani mwake mtume Paulo. Ingawa ni muhimu sisi kuweka wachungaji wakfu kanisani, jambo ambalo ni muhimu zaidi ni sisi kutaka kuwekwa wakfu kwa njia ya kweli na Bwana wetu Yesu Kristo kutokana na upako wake Roho Mtakatifu.



**JE, WAJUA?**


Katikati ya Wayahudi, "Wakati raisi wa sinagogi alipokuwa akiwekwa wakfu, katika kila sherehe kulikuwa na wazee watatu waliokuwa na wajibu wa kumwekea mikono kiongozi huyo mpya. Hii ndio sababu kanuni za mwanzo za Kanisa zilisema kwamba ilibidi kuwe na askofu watatu katika sherehe za kumwekea mikono askofu huyo mpya" [Jamieson-Fausset-Brown, akiongea kuhusu 1 Timotheo 4:14].



## USAWA WA HUDUMA

*"Bali ninyi msiitwe Rabi, maana mwalimu wenu ni mmoja, nanyi nyote ni ndugu. Wala msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni mmoja, aliye wa mbinguni. Wala msiitwe viongozi; maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo. Naye aliye mkubwa wenu atakuwa mtumishi wenu. Na ye yote atakayejikweza, atadhiliwa; na ye yote atakayejidhili, atakwezwa." — Mathayo 23:8-12*

Hata ingawa kuna vipawa tofauti tofauti, na pia kuna wito wa aina tofauti tofauti, na hata kuna usimamizi wa kazi ya Mungu wa aina tofauti tofauti, katika huduma hizo zote kuna usawa wa huduma kati ya wahudumu wote wa injili. Yesu akasema, "Nyinyi nyote ni ndugu." Hapa kwa kweli yeye alikuwa akiongea kupinga vyeo na huduma ambayo inaongozwa kulingana na vyeo. Hata ingawa tunatambua umuhimu wa wachungaji kuwekwa wakfu, na pia kutambua umuhimu wa wao kutumia mamlaka ambayo hupata wanapoweckwa wakfu, mradi mamlaka hayo yanalingana na maandiko, kunao usawa wa kipekee kati ya wachungaji wote katika Kanisa la Mungu.



Yesu aliwaita wanafunzi wake na kuwaambia, "Mwajua ya kuwa wale wanaohesabiwa kuwa wakuu wa Mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha. Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu anayetaka kuwa mkubwa kwenu, atakuwa mtumishi wenu, na mtu anayetaka kuwa wa kwanza wenu, atakuwa mtumwa wa wote" (Marko 10:42-44).

"Hata ingawa vipawa na kuhitimu (kwa kiwango cha hali ya juu) kwa baadhi ya mitume kuliwafanya wao kuwa wa manufaa zaidi katika kazi ya huduma kuliko mitume wengine, jambo ambalo pia liliweka mabegani mwao majukumu makuu zaidi kuliko ya watu wale wengine, kiwango cha unyenyekevu wa wahudumu kutoshana kilidumishwa hadi wakati kanisa lilipoanza kuuacha ukweli" [What the Bible Teaches (Kile Ambacho Biblia Hufundisha), F. G. Smith, uku. 252].

Mafundisho na mazoea ya kuwekwa wakfu kwa wachungaji si jambo ambalo ni kinyume na mafundisho haya ya Biblia, kwa maana wachungaji wa kiungu hufanya bidii ili waweze kuwa na mwelekeo kama ule wa Yesu Kristo, kwa wao kuishi kama kwamba hawana utukufu wowote (Wafilipi 2:5-7) na kwa kufuata mfano ambao tuliachiwa na Bwana wetu. ■

### Je, Kuwekwa Wakfu kwa Mchungaji Ni Jambo Ambalo Hudumu Mpaka Lini?

Kuwekwa wakfu, na pia mamlaka ya kiroho ya mchungaji, ni mambo ambayo hudumu hadi wakati am-bapo mafundisho ya mchungaji huyo na tabia zake zinaacha kuambatana na Maandiko. Kutambulika ambako kunaletwa na mtu kuwekwa wakfu huwa ni jambo ambalo huleta manufaa na linalofanya kazi yake kwa kulingana na jinsi mchungaji huyo anaendelea kufanya kazini mwake ya huduma chini ya upako wake Roho Mtakatifu, huku washirika wake wakiendelea kuwa na imani naye.